Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
Published on *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)

Kutabaruku Kwa Athari Za Mawalii Wa Mwenyezi Mungu Na Kuomba Uponyo

Mawahabi wanaitikadi kwamba kutaka baraka kwenye Athari za Mawalii wa Mwenyezi Mungu ni kumshirikisha Mwenyezi Mungu.

Mawahabi pia wanamuona kuwa ni mshirikina mtu ambaye ataibusu mihrabu ya Mtume [s] na mimbari yake, japo hatafanya hivyo kwa nia ya ibada, isipokuwa ni kwa ajili tu ya mapenzi yake kwa Mtume [s] ndiyo maana katabaruku na kutaka uponyo kwenye Athari zake.

Kukataza kutabaruku kwa athari za Mtume [s] na kulibusu kaburi lake na mimbari yake tukufu ni katika mambo ambayo Mawahabi wametilia nguvu kuyapinga dhidi ya Waislamu, na wamekuwa wakitumia makundi ya askari wa kigaidi waliopewa jina la waamrishaji mema na kukataza maovu, na wamewasambaza (askari) hao katika Msikiti wa Mtume [s] ili wazuwiye kulibusu kaburi lake tukufu na mimbari yake tukufu, pamoja na mihrab ya Msikiti wa Mtume [s].

Mawahabi hawa wanawahujumu mahujaji hapo Madina kwa kila aina ya mateso na kuwazuwiya kutabaruku na kulibusu kaburi la Mtume [s] na utawaona kila mara wameshika fimbo, na mikononi mwao mna nyaya ngumu tayari kumshambulia kila Hujaj atakayethubutu kutabaruku au kulibusu kaburi la Mtume [s].

Na kutokana na hali hii basi, mara kwa mara wamekuwa wakimwaga damu za mahujaji wasio na makosa na kuudhalilisha utu wao katika Msikiti wa Mtume [s], kwa madai kwamba kutabaruku na kulibusu kaburi ni kumuabudu huyo aliyezikwa hapo.

Kwa hakika watu hawa hawaujui Uislamu, na wamekosea kufahamu maana ya Ibada na Maf-humu yake, na kwa sababu hii basi wamepotea njia na wanatangatanga ndani ya upotevu. Wamekuwa wanaona eti kila anapoheshimiwa mtu aliyekwisha kufa ni kumuabudu mtu huyo, pamoja na kufahamu kwamba kubusu kaburi tukufu na kutabaruku kwa athari za Utume siyo kwa ajili nyingine isiyokuwa ya Mwenyezi Mungu, kwa kuwa Waislamu hawamtukuzi Mtume Mtukufu wala hawatabaruku kwa athari

zake ila ni kwa kuwa yeye ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na ni Nabii wake mteule ambaye Mwenyezi Mungu amemtukuza kuliko Manabii wote na viumbe wote.

Basi na ifahamike kwamba kila wanapoheshimiwa na kutukuzwa Mawalii wa Mwenyezi Mungu tendo hilo (kwa asili) ni kumtukuza Mwenyezi Mungu.

Na hauthibitiki ukweli wa Tauhidi ila pale kila kitu kitakapotendwa kiwe ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na katika njia yake, na hapo ndipo itakapokuwa kila kitu kinaanzia kwa Mwenyezi Mungu na kila kitu kinaishia kwake.

Tutazungumzia maana ya Ibada katika sehemu ifuatayo kwa undani, ama sasa hivi utafiti wetu utahusu kutabaruku kwa athari za Mawalii, na utafiti huu tutalazimika kuulekeza kwenye kipimo cha Qur'an na Sunna ya Mtume [s] ili haki iweze kubainika.

Source URL:
https://www.al-islam.org/uchunguzi-juu-ya-uwahhabi-ayatullah-jafar-subhani/kutabaruku-kwa-athari-za-mawalii-wa-mwenyezi-mungu#comment-0